

HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA



Namba ya Kotesheni: LGA.159/2022/2023/W/01

UFUNGUAJI WA BARABARA KWENYE ENEO LA MRADI WA VIWANJA NYAFULA ZENYE UREFU WA KM 59.

MWALIKO WA KOTESHENI

Tarehe: 27/7/2022

1. Mwaliko huu wa Kotesheni unafuata Tangazo la Jumla la Ununuzi (TJU) kwa ajili ya HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA kwa Mwaka 2022/2023 wa fedha.
2. Serikali ya Tanzania imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa kazi za Ujenzi au utekelezaji wa miradi ya HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA katika mwaka wa fedha 2022/2023. Inakusudiwa kuwa sehemu ya fedha hizo zitatumika kugharamia malipo halali chini ya mkataba ambao unatolewa katika mwaliko wa Kotesheni hii.
3. Unaalikwa kuwasilisha Kotesheni yako kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kandarasi za ujenzi kama ilivyoelekezwa kwenye Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi ilivyoainishwa katika sehemu ya pili.
4. Kotesheni zote zijazwe kikamilifu kwa kuanisha Namba ya Kotesheni LGA.159/2022/2023/W/01 ya kazi ya ufunguaji wa Barabara kwenye eneo la mradi wa viwanja Nyafula.
5. Kotesheni zote zikiwa zimejazwa kikamilifu ziwasilishwe Kwa **KATIBU WA BODI YA ZABUNI, HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA S.L.P**

735 MWANZA, kabla ya 01/08/2022 saa 4:00 Asubuhi Siku ya Jumatatu. Ufunguzi wa Kotesheni hizo utafanyika mara baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha Kotesheni.

6. Kotesheni zitatapatikana katika Ofisi ya Ugavi kwa gharama ya Tshs 50,000.00, fedha ambayo hairejeshwi. Na Kotesheni zitatolewa kwa kuanzia saa 1:30 asubuhi mpaka saa 9:30 Alasiri kila siku ya kazi isipokuwa siku za sikukuu.
7. Kotesheni au sehemu ya Kotesheni ambazo zitawasilishwa kwa njia nyingine tofauti zilizowasilishwa katika muundo usiokubalika au baada ya muda wa kuwasilisha kotesheni kuisha hazitakubaliwa wala kuzingatiwa kwa ajili ya tathmini bila kujali mazingira yoyote yale.



SITTA M. SINGIBALA
KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

